



# FAMIS

## Mpango wa Bima ya Afya wa Virginia kwa Watoto

*Ulinzi Wanaostahiki Watoto Wako Kwa Bei Nafuu!*

### Je, FAMIS na Medicaid for Children ni nini?

**FAMIS** ni mpango wa afya ya bima kwa watoto wa Virginia. Huwapa watoto ambao hawana bima ya afya huduma bora za afya. **Medicaid for Children** pia hutoa fidia bora kwa watoto katika familia zilizo na mapato ya chini au zisizo na mapato, hata ikiwa watoto wana bima ya afya. Unapotuma ombi la bima, watoto wako watawekwa kwenye **FAMIS** na **Medicaid for Children**.

### Je, Ni Nini Kinachofidiwa?

- Ziara kwa daktari
- Huduma ya hospitali na dharura
- Uchunguzi wa hali njema yam toto na moto mchanga
- Chanjo
- Dawa za maagizo
- Vipimo na eksrei
- Huduma ya macho na meno
- Huduma ya afya ya akili
- Na zaidi....

Hakuna gharama za kila mwezi wala kila mwaka kwa familia yako iliyo na **FAMIS** au **Medicaid for Children**. Kwa watoto waliosajiliwa katika **FAMIS** pekee, kuna malipo kidogo ya kushiriki (\$2 au \$5) kwa huduma fulani za matibabu.

### Je, Nani Anastahiki?

Watoto wanaweza kustahiki **FAMIS** au **Medicaid for Children** ikiwa:

- Wanaishi Virginia na wana miaka chini ya 19
- Ni raia wa Marekani (wengine ambao si raia pia wanastahiki) Uraia wa mzazi hauzingatiwi
- Wanatimiza vigezo fulani vya mapato (tazama chati ifuatayo)

### Vikomo vya Mapato vya FAMIS (Kabla ya matozo\*)

Ukubwa wa Familia	Kila Mwezi	Kila Mwaka
1	\$2,491	\$29,889
2	\$3,369	\$40,426
3	\$4,247	\$50,963
4	\$5,125	\$61,500
5	\$6,004	\$72,037

*\*Kuanza kutumika tarehe 20 Januari, 2023.  
Vikomo vya mapato vinarekebishwa kila mwaka.  
Piga simu kwa miongozo ya ziada.*

Familia za wahamiaji zilizo na watoto waliosajiliwa hazitawekwa ada ya umma. Kupokea **FAMIS** au **Medicaid for Children** hakutaathiri uwezo wa familia kupata uraia wa Marekani.

### Je, Nitume Ombi Vipi?

Kutuma ombi la **FAMIS** na **Medicaid for Children** ni rahisi.

Piga simu tu ya bila malipo kwa 833-5CALLVA. Wakalimani wanapatikana. Wawakilishi wetu watakuunganisha na mtu anayezungumza lugha unayopendelea.

Au ingia kwenye [commonhelp.virginia.gov](http://commonhelp.virginia.gov) ili utume ombi mtandaoni.

Pia unaweza kutuma ombi kwenye [Department of Social Services](http://Department of Social Services) yako.

Kwa orodha ya nyaraka utakazohitaji unapotuma ombi, tembelea [www.coverva.org](http://www.coverva.org) na ubofye ukurasa wa Tuma Ombi. Utaombwa utoe thibitisho la hali ya uhamiaji wa watoto ikiwa si raia wa Marekani. Ikiwa mtoto wako ni raia wa Marekani, utaombwa utoe nambari ya Ruzuku ya Serikali kwenye ombi.